JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA

WAZIRI MCHENGERWA APONGEZA WAUGUZI, MHUDUMU NA MLINZI KWA KUOKOA MAISHA YA MAMA NA MTOTO

Dodoma: 14 Novemba, 2026

Waziri wa Afya Mheshimiwa, Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) anatoa pongezi kwa Wauguzi, Mhudumu wa Afya na Mlinzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwananyamala ya jijini Dar es Salaam kwa uzalendo, ujasiri na weledi wa kumhudumia mama mjamzito aliyehitaji huduma ya dharura wakati wa kujifungua akishushwa kwenye bajaji.

Taarifa iliyotolewa na wananchi walioshuhudia tukio hilo kwa Waziri Mchengerwa inasema mama huyo mjamzito alifika hospitalini hapo tarehe 13 Novemba 2026 akiwa amechelewa sana hivyo kupelekea kusaidiwa kutoa mtoto akiwa kwenye Babaji ili kuokoa maisha ya mama na kichanga.

Watumishi hao walimkimbilia mama huyo kwa haraka na kumsaidia palepale alipokuwa kwenye bajaji na kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Kwa mujibu wa taarifa ya Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala watumishi waliohusika moja kwa moja ni;

1. Bi. Jestina Mahenge -Muuguzi
2. Bi. Saada Ramadhani- Afisa Muuguzi Msaidizi
3. Bi. Hamisa Daud -Mhudumu wa Afya
4. Bi. Rukia Juma- Mlinzi

Waziri Mchengerwa amewapongeza watumishi hao na kuwazawadia shilingi 500,000/= kila mmoja. Aidha, ametoa wito kwa watumishi wote wa afya nchini kufanya kazi kwa weledi, moyo wa kujitolea wakati wote, hata katika mazingira yasiyotarajiwa.

Imetolewa na;

John Mapepele
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Mji wa Serikali – Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 743
40478, DODOMA

Namba ya Simu: +255 26 2323267
Nukushi No: +255 22 2138060

Barua pepe; ps@afya.go.tz
Tovuti; www.moh.go.tz